

# HALMASHAURI YA MJI KASULU

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



**Simu:** +255282810335  
**Tovuti:** [www.kasulutc.go.tz](http://www.kasulutc.go.tz)  
**Barua pepe:** [td@kasulutc.go.tz](mailto:td@kasulutc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji  
Halmashauri ya Mji Kasulu  
S. L. P 475,  
**KASULU.**

*Unapojibu Tafadhali Taja:*

**KUMB NA.KSTC/S.I/20/52**

**12/11/2020**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI KASULU ANAPENDA KUWATANGAZIA WANANCHI WOTE WENYE SIFA ZA KUOMBA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO:

### 1. MTENDAJI WA MTAI III (NAFASI 1)

#### **Sifa za Mwombaji.**

- Cheti cha Kidato cha IV au VI
- Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya sanaa kutoka chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo-Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **Kazi za Kufanya:-**

1. Mratibu na Mtekelezaji wa sera na sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Mtaa.
2. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu mipango ya Maendeleo katika Mtaa.
3. Mshauri wa Kamati ya Mtaa kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
4. Msimamizi wa utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayohusu uondoaji wa njaa na umaskini katika Mtaa.
5. Kusimamia Ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
6. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote wa Mtaa.
7. Kusimamia Utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo ndogo za mitaa.
8. Na atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
9. Kutekeleza majukumu mengine halali kadri atakavyopangiwa na Mwajiri wake.

#### **MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma TGSB<sub>1</sub> kwa mwezi

#### **Masharti ya kazi.**

Kazi ina masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

## 2. MHUDUMU WA JIKONI /MESS DARAJA LA II (NAFASI 1).

### **Sifa za Mwombaji.**

Awe na cheti cha Kidato cha Nne na uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

### **Kazi za Kufanya:-**

1. Kusafisha vyombo vya kupikia.
2. Kusafisha vyombo vya kulia chakula
3. Kusafisha meza itumiwayo kwa kulia chakula.
4. Kuwatayarishia Wapishi/Waandazi vifaa vya Mpishi na Mezani
5. Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia
6. Kuwasaidia waandazi na Wapishi

### **MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma TGOS A<sub>1</sub> kwa mwezi.

### **MAELEKEZO YA JUMLA NA UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI:**

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri kati ya miaka 18 - 45.
2. Wawe hawajawahi kuajiriwa serikalini.
3. Barua za maombi ziambatishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha Kuzaliwa na Picha mbili (2) za rangi (Passport size) za hivi karibuni. Pamoja na maelezo binafsi (CV).
4. Testimonials, "Provisional Results" Statement of Results" hati za matokeo za kidato cha Nne na sita (Form IV and Form VI Results Slips) **HAVITAKUBALIWA.**
5. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA/NACTE)

### **Namna ya Kuwasilisha maombi:-**

- (i) Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.
- (ii) **Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 26/11/2020 saa 9:30 Alasiri**

### **Maombi yote yatamwe kwa Anuani ifuatayo:-**

Mkurugenzi wa Mji,  
Halmashauri ya Mji,  
S.L.P 475  
**KASULU.**

  
Fatina H. Laay  
**MKURUGENZI WA MJI  
HALMASHAURI YA MJI  
KASULU.**

**MKURUGENZI WA MJI  
HALMASHAURI YA MJI WA KASULU**